*SHULE ZA UMMA ZA SPRINGFIELD - SPRINGFIELD, MASSACHUSETTS*

# FOMU YA ARIFA YA KILA MWAKA YA SHULE YA NYUMBANI

Kwa mujibu wa sheria ya jimbo, hakuna mtoto anayeweza kuanza mpango wa shule ya nyumbani kabla ya kutathminiwa na kuidhinishwa na Msimamizi au mteuliwa. Kwa mujibu wa Sheria ya Jumla ya Massachusetts c.76 § 1, Kamati ya Shule humteua Msimamizi wa Shule kubaini kuwa mpango wa shule ya nyumbani unakidhi viwango vya chini vilivyowekwa kwa shule za umma katika Jumuiya ya Madola ya Massachusetts.

**Maelekezo:** Tafadhali jaza fomu hii kwa ajili ya kila mtoto anayehudhuria Shule ya Nyumbani. Ambatisha hati saidizi na uzitume kupitia barua pepe kwa Ofisi ya Shule ya Nyumbani (Home School Office) kwenye homeschool@springfieldpublicschools.com au utume kwa:

Ofisi ya Mafundisho
Springfield Public Schools
1550 Main Street
Home School Office, 3rd Floor
Springfield, MA 01103

## Tafadhali angalia:

___ Fomu Mpya ya Arifa

___ Fomu ya Arifa ya Kuweka Upya (Tathmini ya kila mwaka ya maendeleo ya kimasomo ya kila mwanafunzi kuanzia mwaka uliopita lazima iwasilishwe pamoja na hati saidizi.)

Je, mwanafunzi huyo kwa sasa anasomea katika Shule ya Umma ya Springfield? ____Ndiyo ___ Hapana
Ikiwa hapana, **wasiliana na Student Assignment Services (SAS)** ili kumsajili mwanafunzi na kuthibitisha ukaaji kabla ya kujaza fomu hii. Tafadhali piga simu kwa SAS kwenye 413-787-6959 ili kuanza mchakato wa usajili.

### Baada ya mwanafunzi kusajiliwa katika Shule za Umma za Springfield, endelea na fomu hii.

Mwaka wa Masomo: __________Nambari ya Kitambulisho cha Mwanafunzi wa Springfield: _____________________

Tarehe ya Kutuma Ombi: __________________ Tarehe inayotakiwa ya kuanza kwa mafundisho ya nyumbani: ___________

## Taarifa ya Mzazi/Mlezi

Jina la Mzazi/Mlezi: _____________________________________________________________

Anwani:________________________________________Zip: __________ Nambari ya simu:_______________

Anwani ya barua pepe ya Mzazi/Mlezi: __________________________________________________________

## Taarifa ya Mwanafunzi

Jina: ___________________________________________________ ____________ ________
Kwanza Kati Mwisho Tarehe ya Kuzaliwa Darasa

Jina la shule ya sasa anayosomea mtoto: ___________________

Je, mtoto wako anapokea Huduma za Elimu Maalum kwa sasa? ______ Ndiyo ________ Hapana

Ikiwa ndiyo, tafadhali ambatisha hati au utoe jina la wilaya ambapo IEP inafanyika. ________________________

**Hati saidizi zinazohitajika: Tafadhali tuma taarifa iliyo hapa chini pamoja na fomu hii kwa Ofisi ya Mafundisho kupitia anwani ya barua pepe ya Home School** homeschool@springfieldpublicschools.com**.**

1. Maelezo ya historia ya kimasomo, uzoefu wa maisha na/au sifa za wale ambao watakuwa wakimfundisha mtoto (kwa mfano tawasifu, historia ya kimasomo, uzoefu wa maisha na/au sifa), jinsi zinavyohusiana na mpango wa mafundisho hapa chini; na

2. Maelezo ya mtaala unaopendekezwa (ikiwemo upeo wa kila somo, malengo makuu, madhumuni na ratiba). Idadi ya saa za ufundishaji katika mtaala unaopendekezwa lazima iwe sawa na angalau saa 900 katika ngazi ya msingi na saa 990 kwa ngazi ya shule ya kati na upili; na
3. Maelezo ya nyenzo za kufundishia na njia za kufundishia zitakazotumika; na
4. Mbinu ya tathmini zitakazotumika kuhakikisha maendeleo ya elimu na kufikiwa kwa viwango vya chini kama ilivyoainishwa na Jimbo la Massachusetts.

Kiungo cha miongozo ya viwango vya Massachusetts kwa ajili ya familia, ambayo hufafanua viwango katika kila darasa kwa kila eneo la somo: https://www.doe.mass.edu/highstandards/default.html

**Tafadhali kumbuka:** Kufikia tarehe 30 Juni, Mzazi/Mlezi anahitajika kuipa Ofisi ya Mafundisho tathmini ya kila mwaka ya maendeleo ya mwanafunzi kimasomo (imeorodheshwa hapo juu). Fomu ya Arifa ya Kuweka Upya yenye hati saidizi kwa ajili ya mwaka wa masomo unaokuja lazima itolewe ikiwa Mzazi/Mlezi anataka kuendelea na Shule ya Nyumbani kwa mwaka wa shule unaokuja.

*Saini ifuatayo inathibitisha usajili wa mwanafunzi na nia ya kutoa kiwango cha chini cha saa 900 za mafundisho katika kiwango cha msingi na saa 990 katika kiwango cha shule ya kati na ya upili. Ninaelewa kwamba ninatakiwa kuarifu wilaya ya shule, kwa maandishi, kuhusu mabadiliko yoyote kwenye anwani ya mwanafunzi ndani ya siku tano (5) za kalenda baada ya mabadiliko hayo kufanyika. Ninaelewa kwamba uidhinishaji huu utategemewa kwa madhumuni ya kuamua ustahiki wa kuhudhuria Mpango wa Elimu ya Nyumbani. Ninathibitisha kwamba ninaweza na ninapoombwa, nitathibitisha taarifa zote zilizotolewa kuhusu ombi hili na kwamba taarifa kama hizo ni za kweli, sahihi na kamili na zimetolewa kwa nia njema.*

**Saini ya Mzazi/Mlezi:**________________________________________________________**Tarehe Iliyowasilishwa**: ______

**Tafadhali kumbuka: Wanafunzi wanaosomea nyumbani hawana haki ya kupata diploma ya Shule za Umma za Springfield baada ya kukamilisha shule ya upili.**

*Tafadhali usiandike chini ya mstari huu

**Kwa Matumizi ya Ofisi Kuu Pekee-Usijaze sehemu iliyo hapa chini**

**Date Received: ____________ Date Accepted: ___________**

**Missing Documents: ____ Yes ____ No**

**Check missing documents:**

_____ Proof of residency
_____ Description of the academic background, life experience, and/or qualifications of those who will be instructing the child (ex. resume, academic background, life experience, and/or qualifications), as they relate to the instruction program below.
_____ Description of the proposed curriculum (including each subject's scope, and major goals and objectives) and schedule. The number of hours of instruction in the proposed curriculum must equal at least 900 hours at the elementary and 990 hours for middle and high school.
_____ Description of the educational materials and instructional methods to be used.
_____ Method of assessment of the child to ensure educational progress and the attainment of minimum standards as outlined by the state of Massachusetts.

**Date Parent/Guardian is given notice of missing documents: ___________________________________**
**Phone: ______________________ Email: __________________________________________________**
**Date of notification to Student Assignment Services (SAS) office: ________________________________**
**Additional comments: ______________________________________________________________________**